

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA AROBAINI NA TATU**

**04 JUNI, 2018**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA TATU – TAREHE 04 JUNI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

### MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

### III. MASWALI:

#### OFISI YA WAZIRI MKUU:

#### 360. MHESHIMIWA DKT. PUDENCIANA WILFRED KIKWEMBE (KAVUU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Serikali imekuwa ikiwahimiza Wananchi wajiunge kwenye vikundi ili waweze kupata mikopo ya kuwasaidia kuendesha shughuli zao:-

Je, Serikali haioni kuwa sharti hilo linawakosesha fursa baadhi ya Wananchi ambao pengine wanahitaji huduma hiyo.

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 361. MHESHIMIWA JOHN PETER KADUTU (ULYANKULU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kabla ya kuanzishwa Shule za Kata, kulikuwa na mpango wa kujenga Shule katika Tarafa. Kwenye Jimbo la Ulyankulu kulijengwa Shule tatu ambazo ni Kashishi, Ulyankulu na Mkindo; Shule ya Kashishi hivi sasa ina Kidato cha Tano na Sita:-

Je, ni lini Shule za Mkindo na Ulyankulu zitapewa hadhi ya kuwa na Kidato cha Tano na Sita ili kuwapunguzia Wanafunzi gharama za kufuata mbali masomo ya Kidato cha Tano na Sita.

**362. MHESHIMIWA MUSSA RASHIDI NTIMIZI (IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Barabara ya Buhekela – Miswaki – Loya – Iyumbu inaunganisha Majimbo ya Igunga, Manonga, Igalula na Singida Magharibi, pia inaunganisha Mikoa miwili ya Tabora na Singida; ina Mbuga kubwa ya Wembele ambapo Wananchi wanalima Mpunga na kulisha Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Singida lakini ni mbovu sana:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuitengeneza barabara hiyo kwa umuhimu wake huo wa kiuchumi na kimawasiliano.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**363. MHESHIMIWA JUMA KOMBO HAMAD (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Mfumo wa ulipaji kodi za kusafirisha



bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umekuwa ukilalamikiwa kwa muda mrefu kwamba unakwaza na kuvunja harakati za biashara Zanzibar na hivyo kusababisha uchumi wa Zanzibar kushuka:-

Je, Serikali ipo tayari kuunda Kamati kwa ajili ya kushughulikia Mfumo wa ulipaji kodi za mizigo kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara.

**364. MHESHIMIWA LUCY MICHAEL MLOWE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Wapo Watumishi katika Sekta ya Afya hususan Madaktari na Wauguzi ambao walijajiriwa katika miaka ya 1980 kupitia Serikali Kuu lakini wakati ule hapakuwepo na makato ya Mfuko wa Kijamii na kuanzia mwaka 1999 Serikali ilianza kuwakata mishahara yao kwenye mfuko wa PSPF:-

Je, Serikali inawafikiriaje Watumishi hao ambao fedha zao hazikukatwa na Mifuko ya Kijamii wakati huo hususan Mfuko wa PSPF.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **365. MHESHIMIWA QAMBALO WILLY QULWI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Matukio ya Wanyamapori kutoka nje ya Hifadhi ya Ngorongoro kwenda katika Vijiji vinavyopakana na Hifadhi hiyo Wilayani Karatu na kuharibu mazao ya Wananchi na kujeruhi watu yamekuwa yakijirudia mara kwa mara:-

- (a) Je, ni nini mkakati wa Serikali kuwadhibiti Wanyama hao ili wabaki katika maeneo waliyotengewa;
- (b) Fidia/kifuta jasho kinachotolewa pindi Wanyama wanapofanya uharifu ni ndogo sana na imepitwa na wakati; Je, ni lini Serikali italeti marekebisho ya kifuta jasho ili kuendana na mazingira ya sasa.

### **366. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Kila mwaka Wanyama waharibifu wamekuwa wanakula mazao ya Wakulima katika Jimbo la Bunda na Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi katika kulipa fidia ya kifuta jasho na kifuta machozi kwa Wakulima hao:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuzuia Wanyama hao wakiwemo Tembo.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**367. MHESHIMIWA FRANK GEORGE MWAKAJOKA (TUNDUMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya Mpemba hadi Ileje kwa kiwango cha lami ili kuunganisha na kuboresha mpaka wa Malawi na Tanzania katika eneo la Isongole.

**368. MHESHIMIWA CATHERINE VALENTINE MAGIGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia Wananchi 55 wa Kata za Oldonyosambu na Mateves Wilayani Arumeru Mkoani Arusha waliopisha ongezeko la barabara ya Arusha – Namanga toka mwaka 2013.



## **WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

### **369. MHESHIMIWA BALOZI ADADI MOHAMED RAJABU (MUHEZA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi zake ikiwemo ya Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni za kutoa maji Mto Zigi kwenda Muheza na Vijij vyake;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani zaidi ya huo wa kuwaletea maji Wananchi wa Muheza.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**DODOMA  
04 JUNI, 2018**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**